**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TANO

## KIKAO CHA SITA

**07 NOVEMBA, 2016**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TANO

## KIKAO CHA SITA – TAREHE 07 NOVEMBA, 2016

**I. DUA:**

**II. MASWALI:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**54. MHESHIMIWA DEOGRATIAS FRANCIS NGALAWA (LUDEWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Pamoja na kwamba Jimbo la Ludewa lina vyanzo vingi vya maji, lakini kuna matatizo makubwa sana ya maji na wadau mbalimbali wamekuwa wakijitokeza kusaidia tatizo hili lakini Serikali na Halmashauri zimekuwa hazitoi ushirikiano kwa kurudi nyuma katika kuchangia sehemu yao kwa kigezo cha kutokuwa na fedha. Mfano Vijiji vya Maholongwa, Mlangali, Mavanga, Manda, Nkomangombe na Lwela:-

(a) Je, Serikali iko tayari kuweka kipaumbele katika kusaidia pale inapohitajika kuchangia;

(b) Je, nini kauli ya Serikali katika kushughulikia tatizo la maji Jimboni Ludewa.

## WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

### 55. MHESHIMIWA HASSAN SELEMAN KAUNJE (LINDI MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:- Sensa ya watu na makazi ya Mwaka 2012 inasema kuwa idadi ya watu katika Jimbo la Lindi Mjini ni takriban 78,000, lakini takwimu za watu waliojiandikisha NIDA inafikia 100,000 na sensa iliyofanywa kupitia Serikali za Mitaa inaonyesha kuwa wakazi wa Lindi Mjini ni zaidi ya 200,000 na Serikali inaendelea kupanga mipango yake ya maendeleo kwa kutumia takwimu za watu 78,000 hivyo kuathiri huduma stahiki za maendeleo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuangalia upya takwimu hizo ili Wananchi wa Lindi Mjini wapelekewe huduma za maendeleo stahiki.

## WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

### 56. MHESHIMIWA RHODA EDWARD KUNCHELA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Tatizo la umeme katika Mkoa wa Katavi hususan Wilaya ya Mpanda Mjini limekuwa kero kwa Wananchi; tatizo hili linafanya maendeleo kuwa duni katika Manispaa ya Mpanda:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuachana na matumizi ya Jenereta ambalo ni bovu linalosababisha ukosefu wa umeme kila mara;

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua kero hii ya umeme.

**57. MHESHIMIWA MARTHA JACHI UMBULLA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Pamoja na juhudi za Serikali kupeleka huduma za umeme Vijijini Wilaya ya Kiteto hasa Kata za Lengatei, Kijungu, Maungu, Songambele, Ndedo na Makame hawajafikiwa kabisa na utaratibu huu wa REA:-

Je, Serikali itapeleka lini umeme katika Vijiji vilivyotajwa.

**WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:**

**58. MHESHIMIWA MASOUD ABDALLAH SALIM (MTAMBILE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi:- Uvuvi ni miongoni mwa Sekta inayochangia pato la Taifa lakini Serikali imekuwa na kigugumizi cha kuboresha Sekta hii wakati tukielekea katika Tanzania ya Viwanda na Uchumi wa Kati.

Je, Serikali ina mkakati gani madhubuti wa kuboresha Sekta ya Uvuvi nchini.

**59. MHESHIMIWA DOTTO MASHAKA BITEKO (BUKOMBE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi:- Wakulima wa Pamba Wilayani Bukombe na Geita kwa ujumla katika msimu wa Mwaka 2015 walipatiwa mbegu na dawa zisizokuwa na ubora ambazo hazikuweza kuua wadudu:-

Je, Serikali inawaambia nini wakulima walioathirika na pembejeo hizo na inachukua hatua gani kuhakikisha jambo hili halijirudii tena.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA MAFUNZO YA UFUNDI:**

**60. MHESHIMIWA ALLY MOHAMED KEISSY (NKASI KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi:- Mhe. Rais alipotuma Waziri wa Ujenzi wakati wa Awamu ya Nne aliahidi kwamba baada ya barabara ya Sumbawanga – Mpanda kukamilika kwa lami atatoa majengo yaliyopo katika Kijiji cha Paramawe Wilayani Nkasi kwa Ujenzi wa VETA, hasa ikizingatiwa kuwa Wilaya haina chuo hicho:-

(a) Je, Serikali iko tayari kutumia majengo hayo kwa ajili ya Chuo cha VETA;

(b) Je, Serikali iko tayari kwenda kuyaona majengo hayo mara barabara itakapokamilika.

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

**61. MHESHIMIWA FREDY ATUPELE MWAKIBETE (BUSOKELO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Halmashauri ya Busokelo ina changamoto za miundombinu ya barabara ambayo hairidhishi na ikizingatiwa kuwa Wananchi wake wanategemea zaidi shughuli za kilimo na usafirishaji wa gesi asilia ya *carbondioxide*:-

(a) Je, ni lini Serikali itajenga barabara inayounganisha Mkoa wa Mbeya na Njombe kupitia Mwakaleli, Kata za Kandete na Luteba;

(b) Je, ni lini Serikali itajenga barabara inayounganisha Jimbo la Busokelo (Kijiji cha Kilimansanga) na Jimbo la Rungwe (Kijiji cha Suma).

(c) Vyanzo vya Halmashauri haviwezi kujenga barabara zote na hivyo kulazimika kuomba msaada TANROADS; Je, ni lini maombi ya Halmashauri ya Busokelo kuhusu kupandishwa hadhi ya barabara zaidi ya tano tulizoomba ili ziwe chini ya TANROADS yatajibiwa.

**62. MHESHIMIWA SEIF KHAMIS SAID GULAMALI (MANONGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Kutokana na majibu ya Mtendaji Mkuu wa SUMATRA Tanzania kutoa maelekezo kuwa mabasi yanayosafiri masafa marefu hutakiwa kusimama katika kituo kimoja ndani ya Mkoa ambako basi hupita, mabasi ya Dar es Salaam - Mwanza yamekuwa yakipita ndani ya Mkoa wa Tabora, katika Wilaya ya Nzega na Igunga na SUMATRA imeteua Nzega kuwa kituo cha kushusha abiria.

(a) Je, Serikali sasa iko tayari kutoa tamko la kuzuia mabasi yatokayo Dar es Salaam Mwanza, Dar es Salaam - Bukoba, Dar es Salaam – Kahama kutokupakia na kushusha abiria yeyote anayeshukia Igunga ili kupunguza ajali za barabarani zinazotokea Igunga;

(b) Je, Serikali inaweza kuruhusu rasmi mabasi yatokayo Tabora pekee kubeba abiria wote wa Igunga ili kupunguza mabasi ya masafa marefu kupakia abiria barabarani.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

**63. MHESHIMIWA FELISTER ALOYCE BURA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Benki ya Wanawake nchini ilianzishwa kwa nia ya kuwasaidia Wanawake kupata mikopo kwa haraka na kwa riba nafuu:-

Je, ni Wanawake wangapi wamekwishanufaika na mikopo ya Benki hiyo kwa Mkoa wa Dodoma.

**64. MHESHIMIWA SILAFU JUMBE MAUFI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Wananchi wamehamasika kujenga Zahanati kwenye Vijiji vyao lakini baadhi hazijakamilika na hata zile zilizokamilika hazijafunguliwa bado na Watumishi nao hawatoshelezi mahitaji; hali hii inasababisha Hospitali za Mikoa ambazo ndiyo za Rufaa kuwa na msongamano mkubwa wa wagonjwa hasa ikizingatiwa kuwa baadhi ya Wilaya hazina Hospitali za Wilaya:-

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya utekelezaji wa kutoa unafuu wa uchangiaji huduma kwa kina

mama wajawazito wanaoenda katika Hospitali za Rufaa;

(b) Je, ni lini Serikali itachukulia afya kuwa ni kipaumbele cha Nchi hasa ikizingatiwa kuwa afya ni kila kitu katika maisha ya Mwanadamu.

**WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

**65. MHESHIMIWA MARIA NDILLA KANGOYE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:- Viongozi wa Dini wanaheshimika sana wanahimiza utulivu na amani na kuliombea Taifa letu. Hata wakati wa kumuapisha Rais Viongozi hawa hupewa nafasi ya kumuombea Rais na kuiombea Nchi:-

(a) Je, ni lini Serikali itatoa umuhimu kwa Viongozi wakuu wa kidini kupewa hadhi ya kupitia sehemu ya Viongozi wenye heshima (*VIPs*) katika viwanja vya ndege na sehemu ambazo kuna huduma kama hizo;

(b) Je, ni vigezo gani au utaratibu gani unaotumika kuwapa Hati za Kidiplomasia watu mbalimbali lakini Viongozi wetu wa kidini hawana hadhi hiyo.

## WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

**66. MHESHIMIWA INNOCENT SEBBA BILAKWATE (KYERWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Wananchi wengi katika Jimbo la Kyerwa wanakabiliwa na tatizo kubwa la upatikanaji wa maji safi na salama, jambo linalorudisha nyuma shughuli za maendeleo:-

Je, ni lini Serikali itatumia maji ya Mto Kagera kuwapatia Wananchi maji safi.

## WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

**67. MHESHIMIWA MARYAM SALUM MSABAHA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Kazi za Vikosi vya Ulinzi na Usalama ni kulinda raia, mali zao pamoja na mipaka ya Nchi lakini kuna baadhi yao wanakwenda kinyume na Sheria kwa kuwapiga Wananchi na kuwasababishia ulemavu au vifo:-

(a) Je, mpaka sasa Serikali imeshawachukulia hatua gani;

(b) Je, mpaka sasa ni Askari wangapi wamekutwa na hatia na kufukuzwa kazi.

**68. MHESHIMIWA PHILIPO AUGUSTINE MULUGO (SONGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itajenga nyumba za Askari Polisi katika Wilaya mpya ya Songwe hasa ikizingatiwa kuwa Maaskari wengi wameripoti ndani ya Wilaya hii mpya.

## III. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

*(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu)*

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2016 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments) (No.3) Bill, 2016).*

**DODOMA**
**07 NOVEMBA, 2016**

**DKT. T. D. KASHILILAH**
**KATIBU WA BUNGE**